LEARNING BY EAR EPISODE – Girls
2nd Episode: Self confidence
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

CHARACTERS:
Anchor: for Intro / Autro
BIBIY.........Main Character.
GRANDMA.........A woman...Adult....with matured voice.
ALMA..........A 15 years. Girl.
ROSSIE..........A 14 or 15 yrs. Girl.

Intro:
Karibu tena kwenye mfululizo wa mchezo wa kuigiza katika makala ya Jifunze Kwa Kusikiliza. Leo hii tunaangazia shida kubwa inayowakabili wasichana..KUTOKUJIAMINI. katika mfululizo wa mchezo wa kuigiza unaosisimua na unaolenga maswala mbali mbali yanayowakabili wasichana.. Leo hii Msichana Bibiy anamuhimiza rafiki yake juu ya umuhimu wa kuondoa uoga na kujenga uwezo wa kuzungumzia shida zinazomkabili.. .Karibu kwenye sehemu ya pili ya Makala ya Jifunze kwa Kusikiliza kwa jina..”Sema Usikike”.

Sign Tune
(sauti za magari yakipita barabarani ... sauti za watu kwenye eneo lenye shughuli za kila siku )

SCENE ONE
(wasichana wawili wanazungumza wakiwa wamekaa kwenye bustani huku sauti za hapo juu zikisikika nyuma yao)

ROSSIE: (akishusha pumzi) Oh Alma, hata sijui ni kwa nini mimi nina tabia ya kuwaacha watu wengine watawale mawazo yangu..yaani nashindwa wakati wote kujimudu mpaka watu waniambie cha kufanya.. kwa mfano nikienda dukani nataka kununuia nguo fulani lakini akitokea mtumwingine aniambie hata hiyo nguo haikufai chukua hii hapa basi mimi mara moja namsikiliza…Alma natamani ningekuwa na uwezo wa kudhibiti

mawazo yangu mie mwenyewe lakini siwezi nimeshindwa kabisa nadhani mimi nina udhaifu Fulani hata sijui nifanyeje.

ALMA: Hey, Rossie, jihadhari rafiki yangu ijapo kuwa binadamu si kamili lakini lazima uwe na msimamo wako wewe mwenyewe pia. Inawezekana labda wewe unapenda kujitia wasiwasi mwingi wa bure maanake dunia hii ukitaka kujua yale yote binadamu wanayoongea juu yako basi lazima rafiki yangu utashikwa na kichaa..mimi siioni sababu yaw ewe kuwa na wasiwasi kiasi hicho.

ROSSIE: Hapana sio hivyo unavyofikiria wewe. Mwenzio hata sijui ni kwa nini najihisi namna hii. kila mara mimi huwa nakata tamaa tu katika maisha saa nyingine nashikwa na aibu, ninakuwa muoga tu bila sababu yaani kila wakati najihisi kuwa watu wananicheka…Alma rafiki yangu labda na huu mwili wangu mkubwa pia unachangia hayo. Najiona sipendezi hata kidogo yaani sina raha hata sijui nifanyeje! Alma.

BIBIY: Enhe wasichana warembo ! What‘s up? Mnaendeleaje na masomo?

ALMA: Aah! Cool tu, isipokuwa Bibiy, huyu rafiki yetu hapa Rossie hana raha hata kidogo na wala mimi sijui nitamsaidiaje yaani ana matatizo kibao.

BIBIY: Hmm... ndiyo hayo? Ana nini rafiki yetu huyu nini hasa kinachomsumbua? Na nini hasa chanzo cha matatizo hayo kibao?

ALMA: Wajua kinachomsumbua zaidi ni kuhusu kutokujiamini au niseme vipi sijui yaani huyu Rossie anajiona hapendezi na mara kwa mara yeye anakuwa anajali sana na kutaka kujua watu wanasema nini juu yake anakuwa na wasiwasi mwingi tu na pia…….

ROSSIE: (Rossie anamkatiza Alma) Aah! Alma, hebu piga breki kidogo. Mimi sikukwambia uanze kutangaza yale

tuliyozungumza sijakwambia wewe uwe ndio msemaji wangu, ujue ukifanya hivyo mimi unanikasirisha na uanazidi kunifanya nijisikie vibaya.

BIBIY: Hebu ngoja kidogo naona hapa kunatatizo kubwa kabisa. Rossie,Sema Usikike.. tafadhali usijidhulumu nafsi yako. C'mon sister, jiamini, jenga hisia za kujiamini na kusanya nguvu za ndani ya moyo wako, jipe muda na ujipe moyo kuwa utaweza. (kwa sauti ya ukakamavu) Angalia Rossie, ukakamavu,ujasiri na kujiamini,... yote haya yanatakiwa uyajenge ndani ya moyo wako na yote yanawezekana kabisa..halafu ndio utakuwa na uwezo kusema kasha usikike.

ROSSIE: Sio rahisi Bibiy. Kwa vyovyote vile hata nikijaribu vipi watu wanafaulu tu kuniingilia kati na kuniumiza mawazo yangu hasa shuleni..nimeshindwa kuelewa ni kwa nini inatokea hivyo?
BIBIY:Unaona sasa umegonga pale pale . (Kimya kidogo)Rossie rafiki yangu Sema Usikike.. Ni nani huyo anayekuumiza kimawazo shuleni?

ROSSIE: Aah! Si kuna huyo mvulana anaeitwa Timo, yeye kila mara huwa ananizomea au ananigoa yaani ananikejeli tu saa zote kwa kweli kijana huyo ananifanya nijisikie kama mtu nisie na umuhimu wowote hapa duniani na hilo ndilo mimi silipendi kabisaaa!.

BIBIY: OK, Rossie mbona hilo ni jambo rahisi kabisa kulitatua.. Wee Mkabili tu huyo jamaa na umwambie yote yale yanayokuudhi ambayo anakufanyia bila kumuogopa. Unasemaje kama unataka kesho mimi nitakuja huko shuleni halafu tumkabili huyu kijana pamoja OK sawa? ama vipi?

ROSSIE: OK Bibiy...sawa niko tayari (kwa sauti ya chini kidogo isiyokuwa na uhakika)

BIBIY: Sawa kabisa Rossie! Changamka wala usisikitike..jamani hebu niacheni niende tutaonana

kesho …Alma kwaherini kwa sasa. (musiki huku Bibiy akiondoka)

ALMA: Wow, Yule ni msichana wa nguvu kweli Rossie Loo! Na zile nywele zake umezionaje, utapenda yaani Bibiy anapendeza kweli looo! mimi huwa ananivutia sana jinsi vile anavyo yakabili mambo kwa kweli hiyo ndio wazungu wanaiita “girl power”. Si umemsikia rafiki yangu Rossie, C'mon changamka usiwe mnyonge mnyonge wala usibabaike rafiki yangu kesho shida yako itakwisha hilo nina hakika... (wote wacheka).twende zetu basi tumekaa hapa kwa muda mrefu kidogo.

MUSIC

SCENE TWO:

BIBIY: Nyanya, hebu niambie kwa nini wasichana wengi wa umri wangu wanakabiliwa na shida ya kutokujiamini?

GRANDMA: kwa nini mjukuu wangu, Enhee una lipi sasa maanake nakujua kipenzi changu Bibiy ukiuliza swali lazima huwa kuna jambo.

BIBIY:Ndio Nyanya ,sababu ninayo ya kuuliza hivyo. Leo nilikutana na rafiki zangu wengine na mmoja kati yao alikuwa na tatizo hilo yaani hana raha anajihisi kuwa yeye hapendezi ana wasiwasi wakati wote na hajiamini kabisa.

GRANDMA: Bibiy mjukuu wangu mimi naelewa ugumu uko wapi hapo najuwa jinsi wasichana wa marika yako wanavyoweza kutumbukia katika matatizo ya aina hiyo kwa sababu hata mimi hapo zamani za kale nami nilikuwa msichana kama hivyo nyinyi. (Soft Music) Wasichana wanapo elekea ukubwani wanachochewa sana na hali ya baadhi ya wanawake au kina mama wanaoishi nao na hasa jinsi wanawake hao wanavyo kabiliana na hali mbali mbali katika maisha yao. Kwa mfano kama wanawake hao wana tabia ya kunyaza tu kila

wakati hata wanapotendewa maovu basi wasichana walio katika mazingira hayo wanafikiri kuwa sio sawa kwa mwanamke kuudhika na jambo lolote atakalo tendewa hata kama sio la haki na kadhalika.

BIBY: Hurray! (anaruka kwa furaha) Asante nyanya. Ndio maana nimemwambia rafiki yangu Rossie kuwa kesho lazima tukamkabili yule kijana anaemsumbua shuleni na amwambie waziwazi kuwa hapendi mwenendo wake!

GRANDMA: Sawa Bibiy pia yataka ufahamu mjukuu wangu kuwa katika miaka yetu ya zamani wanawake hawakuzowea kujieleza hisia zao waziwazi na kwa mtazamo wangu lazima mfumo huo tuukomeshe ili tuwahimize wasichana wetu wajiamini. Umuhimu wa msichana kuwa na uwezo wa kujiamini ni kwamba msichana huyo ataweza kukabiliana na mambo mengi pamoja uwezo wa kufanya maamuzi bora anapohitajika.
BIBIY: Kwa mfano?

GRANDMA: Naam, mfano wasichana wengi wanahofia somo la hisabati wanadhani kuwa hisababti au sayansi ni masomo ya wavulana tu. Na hiyo Bibiy mjukuu wangu inaweza kuwa sababu kubwa ya kuwafanya wasichana washindwe kujiamini vya kutosha kwa sababu kutokujiamini katika masomo hayo na mengineyo kutasababisha msichana asifanikiwe katika ndoto yake maishani.. nasisitiza kuwa wasichana lazima wafutilie mbali mawazo kama hayo na wajue kuwa wao pia wana uwezo kama wavulana unasikia mjukuu wangu.(soft music)Bibiy, wasichana lazima wajenge hisia za kujiamini wakati wote. Uzowefu wa aina hii utawawezesha wasichana kusimama imara dhidi ya mtu yeyote atakae jaribu kuwatendea unyama wa aina yoyote ikiwa ni pamoja na vitendo vya ngono na maovu mengine dhidi ya watoto wa kike.kwa hivyo mjukuu wangu ni muhimu sana kwa msichana anapojiamini.

BIBIY: Lo bibi yangu wewe ndio mambo yote, wewe ndio kisima cha ujuzi. (Kiss) asante Super Granny wangu!
(Bibiy anapiga makofi kwa furaha)

GRANDMA: Hebu ngoja kidogo mrembo wangu mwenye nywele kama Bob Merley mzuri ulieumbika. Kumbuka ni muhimu sana kwa wasichana kupeana moyo na kukumbushana jinsi walivyo warembo. Je wewe ulikumbuka kumwambia rafiki yako kuwa yeye ni mrembo?

BIBIY: Hapana nyanya nilisahau sikumwambia lakini nilimwambia lazima awe imara na asimruhusu mtu yeyote atawale mawazo yake. Nyanya nakuahidi kesho nikimuona nitamwambia kuwa yeye ni mrembo. Bye bye nyanya tutaonana baadae.

GRANDMA: Usiondoke kwanza kabla hujala kitu nenda jikoni nimetayarisha chakula kitamu ule kwanza halafu ndio uende zako.

BIBIY: Asante nyanya.

MUSIC

SCENE THREE
Atmo....(sauti za wanafunzi wakicheza shuleni.....)
ALMA: Hey hebu mwangalieni anakuja malkia wa jangwani mwenye nywele za dredi. Huyo ndie mfano wetu wa yule aliyekuwa mwanamuziki wa Reggie Bob Marley mnamuona!

ROSSIE: Wow! Nakwambia huyu msichana style yake ya nywele ni ya peke yake..hebu mtazame anatembea kwa ukakamavu yaani unamuona jinsi anavyo jiamnini. Alma, nakwambia mimi lazima nitakuwa kama yeye!.. Hi Bibiy, tumefurahi kukuona.

BIBIY: Hi hata mimi nimefurahi sana kuwaona tena. Hey Rossie, unaonekana mwenye furaha sana leo, wow! Hebu tupe siri ya urembo?

ALMA: Bibiy yaani hutaamnini.. Leo Rossie alimkabili yule kijana ana kwa ana na akampasulia yote yaliyokuwa moyoni

mwake..lile somo la jana halikuwa mchezo si unaona amekuwa na ujasiri wa kumkabili peke yake.

BIBIY: Enheeee! Hebu nipashe yaliyotokea!

ROSSIE: Hee unategemea nini Bibiy ? hiyo inaitwa 'Girl Power' yaani nguvu mpya za usichana zilifanya kazi ya ajabu. Oh Bibiy, Nimetambua kwamba ni muhimu kwa msichana kujieleza kinaga ubaga kwa ukakamavu bila woga yaani Yule kijana nilimkabili sio kwa ugomvi bali kwa hekima na kujiamini na nikampasha hadi kesi tukaisawazisha poa kabisa.. na kuanzia hapo ananiheshimu..yaani najisikia raha tele moyoni mwangu.

BIBIY: Hongera dada Rossie.... lazima utambue kuwa hasira za ndani kwa ndani zinaweza kujitokeza nje kwa njia tofauti za kukuathiri maisha yako kwa mfano msichana anaweza kujishtukia tu amebadili kabisa mtindo wa kula manake hasemi kinacho msumbua badala yake anaaza kula hovyo bila mpango, na kibaya zaidi ni pale anapojikuta ameshawishika na kuanza kutumia madawa ya kulevya, Rossie,rafiki yangu tafadhali wape moyo wasichana wenzetu waige mfano wako pia wahimize watambue vipaji vyao na kwa kufanya hivyo itawasaidia sana kujenga hisia ya kujiamini wakati wowote. Rossie,na Alma pia mju inatia moyo sana tukijua kuwa wasichana sisi ni watu muhimu na kila mmoja wetu ni mrembo wa ajabu bibi yangu ameniambia hivyo. Kwa hiyo Rossie usisahau kuwa you are beautiful and very special.

ROSSIE: Hey, asante sana Bibiy nakushukuru kwa maneno yako mazuri.. asante sana umenifanya nijitambue kuwa hata nami ni mtu kati ya watu, kuanzia leo sitakubali tena mtu anivuruge mawazo yangu.

BIBIY: Nina furaha kusikia hayo . (Abadili sauti) Hebu ngojeni kidogo jamani nina wazo nataka kuwaeleza!

ALMA: Enhee unasemaje Bibiy sema usikike tunakusikiliza!!

BIBIY: Naam nadhani nyote mnakumbuka kuwa tulikubaliana kutafuta mbinu zaidi za kukuza uwezo wetu wa kujiamini. Kwa hivyo mimi nafikiri wakati umefika sasa wa sisi kuanzisha mtandao wa Girl Power ambapo kwenye tovuti yetu tutawawezesha wasichana wengi popote walipo kujiunga nasi. tunaweza pia kuanzisha mijadala kuhusu mada mbali mbali na pia kubadilishana mawazo na wenzetu. Mnaonaje wenzangu sote tukiwajibika hata kuchangia malipo ya kwenda kwenye internet Café japo mara moja kwa wiki nafikiri tutafanikiwa kuvumbua mfumo mpya katika kutatua matatizo yetu mabli mbali na la muhimu zaidi tutabadili mtazamo wetu sisi wasichana mnafikiriaje juu ya wazo hilo?

ROSSIE: .....Hilo ni wazo zuri Bibiy, lakini tufanyaje ili kufanikisha hayo yote?

BIBIY: Swali zuri hilo. Kwa mfano katika swala la kujadili mada mbalimbali tunaweza kuwashirikisha wavulana na tuwaalike wazazi wetu kushuhudia mjadala kuhusu maswala ambayo hapo kale yalikuwa ni mwiko kuyazungumzia hadharani kwa mfano Ukeketaji yaani FGM au kuwadhalilisha wasichana au hata pia ukojozi kitandani?

ALMA: .....(anacheka) Oh Bibiy usinivunje mbavu, una maana tusimame mbele ya umati wa watu na kuanza kuzungumza juu ya kukojoa kitandani? Sidhani kama hilo ni tatizo kubwa linalohitaji mjadala.

BIBIY: Hata kidogo Alma hilo sio jambo la kucheka nyanya yangu ameniambia kuwa hii ni shida kubwa kabisa ambayo vijana wengi hawataki tu kusema wazi wazi kuwa wanakabiliwa na shida hii ya kukojoa kitandani lakini ameniambia kuwa tatizo hili linaweza kutibiwa hospitali.

ROSSIE: Ni kweli Bibiy, Nafikiria unayoyasema ni kweli. Mimi nakuunga mkono moja kwa moja wala sina pingamizi.

ALMA: Hata mimi pia naunga mkono wazo lako Bibiy.

BIBIY: OK sasa basi tuinue mikono yetu kama kawaida tuombe sala yetu ili wazo letu lifanikiwe.

Pamoja tunasimama,
Pamoja tunakata kauli,
Sasa na siku za usoni,
Kuushinda udhaifu,
Wa kutojiamini.

MUSIC

Aturo: Naam msikilizaji wasichana wameamua kuanzisha mtandao wa Girl Power na pia wamekata kauli kupambana na udhaifu wa kutokujiamini. Na mpaka hapo ndio tumekamilisha sehemu ya pili ambapo leo hii mchezo wetu wa kuigiza katika makala ya Jifunze kwa Kusikiliza umegusia umuhimu wa kujiamini kwa wasichana. Unaweza kuusikiliza tena mchezo huu wa hadithi au mwambie rafiki ausikilize kupitia kwenye tovuti yetu HYPERLINK "http://www.dw-world.de/lbe" www.dw-world.de/lbe Je ni kipi kitakacho tokea katika sehemu ya tatu ya mchezo wa hadithi katika makala ya Jifunze Kwa Kusikiliza usikose kujiunga nasi wiki ijayo wakati msichana Bibiy anapounda hicho kikundi cha girl power network, hadi wakati huo Kwaheri.

END